

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَكَلُوا الصَّدِيقَاتِ لِيَسْتَخْفَتُهُنَّ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَمْ يُكَفِّرُنَّهُنْ دِيَنَهُنَّ الَّذِي أَنْقَعَ لَهُنْ وَلَمْ يُبَدِّلُنَّهُنْ مِنْ بَدْلِهِنْ هُنْ أَنَّهَا
يَعْبُدُونِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُنُ الظَّاغِنُونَ



Alhamisi, 14 Sha'aban 1446 H

13/02/2025 M

Na: HTS 1446 / 49

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari
Wanasiasa wa Sudan Wanatekeleza Njama za Amerika Kuichana Nchi!
(Imetafsiriwa)**

Mnamo Alhamisi, 13 Februari 2025, Al-Sharq iliripoti kwamba Osama Saeed, kiongozi wa Chama cha Mapinduzi, alisema: "Kundi letu linapanga kutangaza serikali kufikia mwisho wa Februari." Alikuwa anakusudia serikali sambamba na ile iliyopo Port Sudan kwa sasa. Alifafanua zaidi: "Ngazi za utawala katika serikali ya kiraia ndani ya maeneo yanayodhibitiwa na Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF) zitajumuisha rais wa Baraza Kuu, wajumbe, na Baraza la Mawaziri."

Msisitizo wa baadhi ya wanasiasia—ambao hapo awali walikuwa sehemu ya muungano wa Taqaddum—kuanzisha serikali sambamba na utawala wa Al-Burhan mjini Port Sudan, hasa katika maeneo yanayodhibitiwa na RSF, unakuja wakati ambapo jeshi linasonga mbele na kuyalinda maeneo makubwa ya Al-Jazeera, Khartoum, na kwengineko. Wakati huo huo, vikosi vya RSF vinaelekea Darfur, ngome yao, ambapo tayari wanadhibiti sehemu nne kwa tano za eneo hilo, huku Darfur Kaskazini pekee ikisalia nje ya udhibiti wao. Ni katika maeneo haya kwamba Osama Saeed na wanasiasia wengine wanaonekana kuwa na nia ya kuanzisha serikali, na kufanya Darfur mgombea mkuu wa kujitenga – kama vile Sudan Kusini ilivyofanya. Hii inaendana na mpango wa muda mrefu wa kikoloni.

Na cha kusikitisha ni kwamba, haya yanatendeka mikononi mwa wana haswa wa nchi hii yenyе taabu—wanasiasia wabinafsi ambao ni vibaraka wa wakoloni makafiri wa Magharibi. Wanatekeleza mradi wa Bernard Lewis, mwanahistoria wa Kiyahudi wa Marekani anayejulikana kama "muuaji wa Mashariki ya Kati," ambaye alipigia debe mgawanyiko zaidi na kugawanywa kwa ardhi za Kiislamu kwa misingi ya kikabilo, madhehebu, na kikanda. Katika kikao cha siri mwaka 1983, Bunge la Congress la Marekani lilipitisha ruwaza ya Bernard Lewis, ambapo Marekani inataka kuigawanya Sudan katika dola tano tofauti, kama Rais wa zamani Omar al-Bashir alivyotaja katika mojawapo ya mahojiano yake na vyombo vya habari.

Kupitia Al-Bashir na wanasiasia wengine, Amerika ilifanikiwa kuitenganisha Sudan Kusini kupitia Mkataba muovu wa Naivasha. Sasa, ni inajitahidi kuitenganisha Darfur kupitia kwa wanasiasia ambao wamemsaliti Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na waumini—wanaouza dini yao kwa ajili ya manufaa ya kidunia ya wengine!

Sisi katika Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan hapo awali tulionya dhidi ya kutenganishwa kwa Sudan Kusini na tukawasihi watu wa Sudan kufahamu njama za wakoloni makafiri za kuichana nchi yetu. Sasa, tunafichua mpango wa kuitenganisha Darfur kabla haujatokea. Tunatoa wito kwa watu wenye ikhlasi wa nchi hii kutong'atwa mara mbili kutoka kwenye tundu moja. Tunawataka wasimame kidete dhidi ya njama za dola za kikoloni za Magharibi, hususan Marekani, na kuwazuia wanasiasia hao ambao wamejitia katika mikono ya ubeberu na wanatekeleza njama zake dhidi ya ardhi yetu.

[إِنَّمَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَحْيِبُوا إِلَهٌ وَلِلَّهِ رَسُولٌ إِذَا دَعَاهُمْ لِمَا يُحِبِّبُكُمْ]

"Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele." [Al-Anfal:24].

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)
Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir katika Wilayah Sudan**